# MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

•

**SWALI LA KWANZA**

- Mtahiniwa azingatie muundo rasmi wa kumbukumbu.

(i) Kichwa kionyeshe wanaokutana
- (chama cha Kiswahili)
- Mahali mkutano unapofanyika mfano ukumbini.
- Tarehe na saa ambapo mkutano kafanyika.
- Kichwa kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe msitari.

(ii) Orodha ya watu izingtie:-
- Wanachama waliohudhuria kwa kuzingatia itifaki.
- Wanachama waliotuma udhuru.
- Wanachama ambao hawakuhudhuria wala kutuma udhuru.
- Idadi ya wanachama waliotuma udhuru na waliokosa kuhudhuria isiwe zaidi ya robo ya waliohudhuria.
- Iwapo kuna mgeni jina lake liandikwe katika mahudhurio / mwalikwa

(iii) Mtahiniwa aorodheshe ajenda: Mfano

(a) Kufunguliwa kwa mkutano

(b) Kusoma na kuthibitishwa kwa kumbukumbu.

(c) Masuala kutokana na kumbukumbu hizo mikakati.

(iv) Hojai

(i) Kuandaa warsha na kongamano

(ii) Kutaka siku za kuzungumza Kiswahili.

(iii) Kuandaa mijadala.

(iv) Kufungua maktaba shuleni.

(d) Masuala mengineyo / shughuli

(e) Kufunga mkutano / kumalizia

Mtahiniwa afafanue kila hoja kama kumbukumbu inayojisimamia kwa mkato na urasmi.

(f) Katika sehemu ya thibitisho mtahiniwa awache nafasi zile zikiwa wazi
Mwenyekiti………… Tarehe …………………. Sahihi ……………..
Katibu ……………… Tarehe……………………

(g) Mtahiniwa azingatie uakifishaji mwafaka na istilahi maalum.

**<u>SWALI LA PILI</u>**

❖ Mtahiniwa azingatie insha ya mjadala ambayo itaonyesha pande mbili (kuunga na kupinga)

Mtahiniwa anaweza akaunga kauli mkono kwa kutoa hoja mahususi na kuzifafanua ipasavyo.

Iwapo atapinga vile vile atoe hoja zitakazothibitisha msimamo ule.

Mtahiniwa ahitimishe kwa kuchukua msimamo kwa kuegemea upande ulio na hoja nyingi.

Mfano wa hoja za kuunga mkono

(i) Utalii umechangia visa vya kuzorota kwa usalama / ughaidi

(ii) Utalii umeathiri maadili kwa njia hasi.

(iii) Utalii umechangia biashara haramu – Uuzaji wa mihadarati
-Uwindaji haramu

<u>Kupinga</u>

(i) Utalii ni mojawapo ya nguzo za uchumi hivyo basi huchangia maendeleo.

(ii) Utalii huchangia umoja na utangamano: Miongoni mwa jamii tofauti nchini.

(iii) Huhifadhi, hukuza na kustawisha utamaduni wetu kama taifa.

(iv) Utalii huwawezesha watu kuyajua mazingira na taifa lao kwa jumla.

(v) Utalii umechangia uimarishaji wa miundo msingi na usalama katika taifa.

(vi) Utalii umechangia nafasi nyingi za ajira.

(vii) Utalii umechangia kuimbuka kwa Viwada/Biashara/Taasisi badala mfano hoteli, uchukuzi

Mtahiniwa azingatie sarufi ipasavyo:
- Tahajia mwafaka
- Uakifishaji unaofaa
- Miundo ya sentensi na mpangilio wa maneno.

Mtahiniwa aandike hoja zake kwa namna iliyo na mtiririko na kukuza aya kamili.

**SWALI LA TATU**

- Hii ni insha ya methali.
- Mtahiniwa aandike kisa kitakachooana na maana ya ndani na vile vile maana ya juu juu.
- Mtahiniwa azingatie sana maana ya ndani bila ya kupotoka katika kisa chake.
- Mtahiniwa atumie kisa kinachoaminika hata kama ni cha kubuni.
- Insha itakayo andikwa idhihirishe pande zote mbili za methali.
- Mtahiniwa ateue lugha yenye mvuto na msamiati mwafaka.
- Ni sharti kisa chake kiwe na mtiririko mzuri wa mawazo na mantiki.
- Mtahiniwa azingatie sarufi ipasavyo.
- Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa njia mwafaka. Hili lawezekana kwa kukariri methali ile au kutumia nyingine iliyo na maana sawa.

**SWALI LA NNE**

(i) Hii ni insha ya mdokezo.

(ii) Mtahiniwa aandike kisa ambacho kitamalizia kwa kuoana na kauli iliyotolewa.

(iii) Mtahiniwa aipe insha yake kichwa mwafaka.

(iv) Kisa kile kiwe na maudhui yaliyofafanuliwa kwa njia iliyo na mantiki.

(v) Mtahiniwa aonyeshe ubunifu wa hali ya juu na ataeue msamiati ipasavyo.

(h) Mtahiniwa vile vile azingatie sarufi ipasavyo -
- Tahajia safi
- Mpangilio wa maneno
- Miundo ya sentensi

(i) Mtahiniwa azingatie urefu wa insha.

(j) Mtahini akadirie kisa kilichotolewa na mtahiniwa kwa mjibu wa mdokezo uliotolewa.